



CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA CHA JARAMOGI OGINGA ODINGA

KITIVO CHA ELIMU

MTIHANI WA CHUO KIKUU MWAKA 2017/2018

MWAKA WA PILI MUHULA WA KWANZA

MAIN CAMPUS REGULAR

NAMBA YA KOZI: ESN 2212

KOZI: KISWAHILI

CHUMBA CHA MTIHANI:

KIKUNDI: DIP. SNE

TAREHE:

WAKATI:

MUDA: SAA 1 ½

MAAGIZO

1. Jibu swali la kwanza (**LAZIMA**) na maswali mengine yoyote mawili.
2. Watahiniwa wanashauriwa wasiandike kwenye karatasi ya maswali.
3. Watahiniwa sharti wamkabidhi msimamizi wa mtihani karatasi za majibu wakiwa ndani ya chumba cha kufanya mtihani.

SWALI LA KWANZA

a) Eleza dhana zifuatazo:

- | | |
|--|-----------|
| i) pijini | (alama 3) |
| ii) lugha ya mama | (alama 2) |
| iii) lugha ya kwanza | (alama 2) |
| iv) sheng | (alama 2) |
| v) kuchanganya ndimi | (alama 2) |
| vi) kielezi | (alama 1) |
| b) i) hadithi | (alama 2) |
| ii) taja sifa mbili za nomino katika ngeli ya A-WA | (alama 2) |
| iii) eleza maana tatu tofauti ya neno PAAkatika sentensi. | (alama 4) |
| c) Msichana wa Bwana Asuma anayeitwa Nambolwa, aliolewa na mvulana wa Achieng, kwa jina Okere. Awuor ni dada yake Asuma, na Betty ndiye kitinda mimba katika familia hiyo. | |
| i. Asuma na Achieng wanaitana vipi? | |
| ii. Mtoto wa Asuma anamwitaje Betty? | |
| iii. Awuor na mke wa Auma wanaitana vipi? | |
| iv. Ni jina gani mtoto wa Betty atamwita Yule wa Achieng? | |
| v. Taja neno jingine badala ya: | (alama 5) |
| a) Mtu | |
| b) msichana | |
| c) kibonzo | (alama 3) |
| v) Taja ugonjwa unaosababishwa kwa kung'atwa na mbung'o | (alama 1) |
| vi) Msimu wa mvua nyingi huitwaje? | (alama 1) |

SWALI LA PILI

- | | |
|--|------------|
| a) Thibitisha kauli kwamba Kiswahili ni Kibantu | (alama 8) |
| b) Eleza mambo yanayozingatiwa katika kuisanifisha lahaja fulani ili itumike kama lugha. | |
| | (alama 12) |

SWALI LA TATU

- | | |
|---|------------|
| a) Eleza sifa zinazobainisha sajili ya biashara. | (alama 12) |
| b) Kwa kutoa mifano, | |
| i) tofautisha lahaja na lafudhi | |
| ii) tofautisha fasihi andishi na fasihi simulizi. | (alama 8) |

SWALI LA NNE

- | | |
|--|------------|
| a) Eleza aina zozote tano za nomino, huku ukitoa mfano kwa kila aina | (alama 10) |
| b) Kama mwalimu wa Kiswahili katika shule ya msingi, ni matatizo gani yatakukumba utakapokuwa nyanjani kufundisha? | (alama 10) |

SWALI LA TANO

- a) Andika wingi wa sentensi zifuatazo:
- i) Mama alianua nguo yake baada ya kutoka sokoni. (alama 2)
 - ii) Mtoto alipojaribu kukata waya, umeme ulimrusha chini. (alama 2)
- b) Changanua sentensi hizi kwa njia ya matawi:
- i) Yule mwanafunzi mdogo amefaulu. (alama 2)
- c) Andika katika usemi wa taarifa:
- i) Mwalimu aliwaamuru wanafunzi wote waingie darasani mara moja. (alama 2)
- d) Nyambua vitenzi hivi katika kauliya kutendesha:
- i) panda
 - ii) nywa (alama 2)
- e) Katika sentensi ifuatayo, tambua vivumishi viliviyotumika na ueleza ni vya aina gani?
- i) Niliona kile kitabu chekundu cha mwanafunzi wangu kimeraruka. (alama 4)
- f) Eleza aina ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hizi:
- i) Mtu yeyote anayetaka kuchukua ambacho si chake, ni mwizi. (alama 2)
- g) Andika kinyume:
- i) Baba alikichoma kisu ukutani kasha akakunja nguo alizoanika mchana. (alama 2)
- g) Kanusha:
- i) Samahani, nitakusahau. (alama 2)